COMPETENCY BASED CURICULUM SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 2 TERM 1 EXAMS 2023

MASWALI

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
Mwalimu aulize maswali. Mwanafunzi ajibu kwa sauti.

1. Bendera ya nchi yetu ina rangi ngapi?
   Mwanafunzi ajibu.
2. Taja rangi moja inayopatikana kwenye bendera yetu.
   Mwanafunzi ajibu
3. Taja siku ambazo bendera hupandishwa juu.
   Mwanafunzi ajibu
4. Bendera inapopandishwa watu wanaimba wimbo upi?
   Mwanafunzi ajibu
5. Taja majina ya raisi wa nchi ya Kenya.
   Mwanafunzi ajibu

KUSOMA KWA SAUTI
Soma hadithi ifiuatayo kwa sauti
Leo ni siku ya Jumapili. Tunajitayarisha kwenda kanisani na watu wa familia yangu. Nimevaa mavazi ya rangi ya samawati na shati jeupe. Nimevalia soksi za rangi nyeusi. Mama yangu anataka nivae viatu vyangu vipya. Baba ndiye alininulia viatu hivyo. Baba amevaa suruali ndefu na shati ambalo ni ya rangi sawa na yangu. Amejifunga tai shingoni. Mimi na baba tumevaa mavazi yanayofanana.
Mama amevaa rinda la rangi nyekundu. Yeye anapenda rangi nyekundu. Amevaa viatu vinavyomotamota. Anapendeza sana. Kila siku ya Jumapili sisi huhudhuria ibada kanisani. Huwa tunavaa mavazi yetu yanayopendeza.

UFAHAMU
Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali.
Mimi ninaitwa paka. Mimi pakasipendi uchafuchafu hufanya umbo lisokote. Mimi hujifuta mikono kila mara. Sirambi kucha zangu ovyoovyo. Huwa nasafisha kucha zangu vizuri. Ninapenda usafi. Ninapotaka kujisaidia ninachimba shimo. Nikimaliza kujisaidia ninalifunika. Nina kazi nyingine muhimu sana kwa binadamu. Mimi hufukuza panya nyumbani. Panya huharibu nguo za binadamu na mahindi waliyovuna. Binadamu hunipatia maziwa kwa kazi yangu nzuri. Mimi hufurahia kazi hiyo.

Maswali

1. Paka anapenda nini?